**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**UTEKELEZAJI NA MAFANIKIO YA SHUGHULI ZA SERIKALI MKOA WA ARUSHA JANUARI HADI DISEMBA 2017**

**UTANGULIZI**

Mkoa wa Arusha ni moja kati ya Mikoa 26 ya Tanzania Bara, wenye ukubwa wa Km za mraba 34,515.5. kiutawala Mkoa unao Wilaya sita Halmashauri 7, Tarafa 23, Kata 33, Vijiji 393, mitaa 154 na vitongoji 1471.

Idadi ya watu kwa ongezeko la 2.7% kwa mwaka inakadiriwa kufikia jumla ya watu wapato 1,835,787 wanawake wakiwa 51.5% na wanaume 48.5%.

**UCHUMI**

Shughuli za kiuchumi katika Mkoa wa Arusha hasa hasa za kilimo na wafugaji ambao huchangia 20%, biashara huchangia 10.9%, viwanda na sekta nyingine huchangia 15.5%.

Pato la Mkoa limefikia Tsh. Trilion4,876, ambalo huchangia asilimia 4.77 kwenye pato la Taifa. Pato la Mkoa kwa mwaka ni (per capital income Tsh. 2,576.517).

**HALI YA USALAMA**

Hali ya ulinzi na usalama ya Mkoa ya Mkoa wa Arusha ni ya kuridhisha hasa baada ya juhudi kubwa kuwekwa na vyombo vya ulinzi na usalama kudhibiti mianya ya matuko yanayosababisha uvunjivu wa Amani. Wananchi wameendelea na shughuli za uzalishaji mali na kukuza kuhusu bila hofu yoyote ya usalama wao wa mali zao.

**TAARIFA ZA SEKSHENI NA VITENGO**

## 1.0. SEKSHENI YA UTAWALA NA RASILMALI WATU

## MAFANIKIO

1. Imeweza kufanya Mafunzo kwa Maafisa Utumishi wote wa Halmashauri na Taasisi zipatazo **22** ambapo Maafisa **48** walipewa Mafunzo kwa undani kuhusu Sheria na taratibu za kuchukua kuhusu mashauri ya Kinidhamu, wamejifunza kuhusu kupima Utendaji kazi wa wazi OPRAS na wamejifunza kuandaa **bajeti** ya mishahara ambayo huko nyuma hawakuwahi kupata mafunzo hayo.

2. Seksheni imewezesha watumishi **39** kwenda masomoni kwa kada mbalimbali na hasa za afya kwa masomo ya muda mrefu.
3. Seksheni katika kusimama ustawi wa watumishi wake imetoa mafunzo na upimaji wa afya kwa watumishi wa RS na MSM wote kwa kupimwa magonjwa sugu yasiyoambukiza na virusi vya ukimwi jambo ambalo limefanyika kwa ufanisi.

4. Seksheni imeweza kuendesha mafunzo kwa Maafisa Utumishi ambapo mada ziliwasilishwa na Wataalamu toka Ofisi ya Rais Utumishi. Mafunzo haya yamekuwa dira kwa Maafisa Utumishi.

5. Seksheni imeweza kusimamia, na kuratibu, ziara mbalimbali za kikazi za viongozi, za ndani na nje ya Mkoa na hata nje ya Nchi, hasa za Mheshimwa Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa pamoja na viongozi na watendaji wengine.

## 2.0. SEKSHENI YA UCHUMI NA UZALISHAJI MALI

### Sekta ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji

Mkoa wa Arusha ni moja ya Mikoa iliyopiga hatua kubwa katika maendeleo ya viwanda hapa nchini. Kuna Viwanda Vikubwa 38, vya Kati 131 na Vidogo 2165 vinatoa ajira zaidi ya 50,000 na vinachangia asilimia 10.9 ya pato la Mkoa.

Kwa kipindi cha miaka miwili yaani 2016/2017 na 2017/2018 - Mkoa unajumla ya Viwanda 35 vipya vilivyo katika hatua mbalimbali ambavyo vinakadiriwa kutoa ajira kati ya 600 hadi 700. Aidha Mkoa kupitia Halmashauri zake umetenga maeneo ya ekari 77,110 kwa ajili ya Uwekezaji. Kati ya hizo ekari 4100 zimeanza kufanyiwa mpango wa kupimwa viwanja 171 kwa ajili ya viwanda na uwekezaji katika eneo la Malula halmashauri ya Wilaya ya Meru na Wasso Ngorongoro.

### Sekta ya Kilimo
### Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhi Vitunguu Karatu.

Serikali kupitia Programu ya MIVARF imejenga ghala la kuhifadhi vitunguu kwa ajili wa wakulima wa zao hilo pamoja na miundombinu ya ya barabara

katika Tarafa ya Eyasi, Wilaya ya Karatu. Mradi huo umegharimu jumla ya Shilingi za kitanzania 1,530,450,036/- ambayo asilimia 95 ni ya Mradi na asilimia 5 ni ya Halmashauri ya Wilaya ya Karatu uwezo wa kuhifadhi vitunguu hadi tani 2400.

Mradi huu tayari umekamilika na tayari wakulima wote wanaendelea kuhifadhi vitunguu na kuanzia tarehe 1/12/2017 shughuli zote za biashara ya vitunguu zimeanza kufanyikia ndani ya eneo la Ghala hilo kama soko pekee kwa ajili ya kuendeshea shughuli ya biashara ya vitunguu.

Wakulima wameishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kondoa kero iliyodumu kwa muda mrefu ambapo kulikuwa na wavamizi kutoka Nchi jirani katika mashamba yao ambapo walikuwa wakinunua mazao yangalipo mashambani kwa bei waliyoamua wao. Tangu kujengwa kwa mradi huo, bei ya vitunguu imeongezeka kutoka TSh. 40,000 Kwa gunia hadi Tsh 100,000 kwa gunia baada ya mradi, baada kuhifadhiwa katika ghala hilo na kuuzwa katika soko halali linaloendeshwa eneo hilo la ghala.

Pamoja na mafanikio Serikali imegundua bado kuna matumizi yasiyo sahihi ya vipimo hivyo inahitajika kutoa elimu ya matumizi sahihi ya vipimo ili wakulima wasiendelee kupunjwa na Serikali kukosa mapato halali

**Sekta ya Mifugo**

**Ujenzi wa Soko la kisasa la mifugo**

Ujenzi wa Soko la kisasa la mifugo katika Kijiji cha Eworendeke Wilayani Longido ambalo lipo kwenye hatua za mwisho za ujenzi chini ya Programu ya MIVARF. Ujenzi huu umegharimu kiasi cha Tsh. 782,050,572 ambayo asilimia 95 ni ya Mradi na asilimia 5 ni ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido. Uwepo wa Soko hili utasaidia kupunguza kero ya utoroshwaji wa mifugo kwenda Nchi jirani, kuongeza uzalishaji wa Mifugo na mazao yake kutokana na uwepo wa uhakika wa soko la mifugo. Pia kuboresha na kuinua kipato cha wananchi kwa kuuza mifugo ndani ya Tanzania na Nchi jirani, ajira kwa vijana na wanawake pamoja na kuipatia Serikali mapato ambayo yalipotea kwa muda mrefu kutokana na utoroshwaji wa mifugo kwenda nchi jirani.

Aidha, uwepo wa soko hili utasaidia kuhifadhi mazingira yaliyokuwa yanaharibiwa na mifugo waliokuwa wakitoroshwa kwa kuswagwa kupitia njia zisizo rasmi kwenda Nchi jirani.

## Sekta ya Maliasili Na Utalii Na Uhifadhi Wa Mazingira

### Kuondolewa malango 'Gates' ukanda wa ziwa Natroni

Sekta ya Utalii imekumbwa na changamoto ya muda mrefu wa uwepo wa Mageti katika ukanda wa Ziwa Natroni ambapo mageti yalikuwa yamewekwa kila mpaka wa Halmashauri za Wilaya ya Monduli, Longido na Ngorongoro. Mwaka 2017/2018 Mkoa kupitia Mhe. Mkuu wa Mkoa umefanya jitihada za Kuhakikisha keKuondolewa malango 'Gates' matatu ambayo yalikuwa kero kwa wageni "Tourists" mwelekeo wa ukanda wa Ziwa Natroni katika Halmashauri za Wilaya ya Monduli, Longido na Ngorongoro. Baada ya jitihada mbalimbali yalifikia kubakisha lango moja linalokusanya mapato kwa ufanisi.

Kumekuwa na ongezeko la wageni/watlii wanaotembelea vivutio (***"Number of Visitor Arrivals***") ambapo mwaka 2016 watalii 1,284,279 na "projection" kwa mwaka 2017 ni 1,436,480 na inatarajiwa kuongezeka. Aidha, asilimia 80 ya Watalii wanaofika Tanzania hufika/kupita Mkoa wa Arusha.

Mapato yatokanayo na Utalii yamekuwa yakiongezeka kutoka trilioni 3.71 mwaka 2015 hadi trilioni 4.64 Mwaka 2016; Aidha, mapato yanakadiriwa kuongezeka kwa kulinganisha mapato ya mwezi Januari – Novemba, 2017 NCAA na TANAPA pekee, Jedwali Na. I: limeainisha takwimu za mapato kitaifa kwa mwaka 2015 & 2016 na mapato ya Januari - Desemba, 2017 ya NCAA na TANAPA. Mapato mengine ya Utalii yanatokana na Utalii wa Picha, Utalii wa Uwindaji na Utalii wa Utamaduni na (WMA).

***Jedwali Na. I: Takwimu za mapato kitaifa kwa mwaka 2016 & 2017, pia mapato ya Mwezi Januari – Novemba, 2017 kwa upande wa NCAA na TANAPA.***

| MWAKA | MAPATO KITAIFA | TANAPA | NCAA |
|---|---|---|---|
| 2016 | Trilioni 4.64 | - | - |
| Januari-Novemba, 2017 | - | 138.7bilioni | - |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Januari -  , 2017 | - | - | 65.6bilioni |
| 2015 - 2016 | Ongezeko; **Bilioni 87** | - | - |

***Chanzo:*** *Kitabu cha Takwimu za Utalii cha Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Utalii, Mwaka 2016 ; NCAA & TANAPA, 2017*

## Mradi wa Kukabilinana na Mabadiliko ya Tabia Nchi

Kwa muda wa zaidi ya Mikaka 10 Mkoa wa Arusha umekwa ukikabilia na mtawanyiko hafifi ambao umesababisha upungufu wa maji,  malisho na na hata kusababisha mifugo kufa na upungufu wa uzlishaji wa mazo ya chakula na biashara. Serikali kwa kushikiana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali IIED na Hakikazi Catalyst wametekeleza kwa kasi Miradi 34 ambayo inagharimu Tsh. 1,908,015,342 kwa ajili ya kukabiliana na Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabia Nchi katika Halmashauri Za Wilaya za Longido, Monduli na Ngorongoro**.**

## Baraza la Uwezeshaji

## Mafanikio ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Katika Mkoa Wa Arusha Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Makundi ya Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu ni muhimu katika ujenzi wa Taifa letu hususan katika Nyanja ya uchumi. Ili kufikia uchumi wa kati unaotegemea tasnia ya viwanda Serikali ya Awamu ya Tano imefanikiwa kuongeza makusanyo ya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hali iliyopelekea ongezeko kubwa la idadi ya Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu kunufaika mikopo ya **10%** inayotengwa kwenye makusanyo ya ndani. Aidha, uwezeshaji kwa vijana, wanawake na wenye ulemavu katika mwaka wa fedha 2016/2017 kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa ni jumla ya **Tshs. 2,554,500,000/=** kwa vikundi **279** vya vijana na vikundi **370** vya wanawake. Ambapo vijana **Tshs. 1,059,000,000/=** na wanawake **Tshs. 1,495,500,000/=** ikiwaazma kubwa ni kuongeza ushiriki wa shughuli za kiuchumi na uzalishaji mali katika makundi haya muhimu ya ujenzi wa Taifa.

Mkoa unaendelea kumuunga mkono Mhe. Mama Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, juhudi za kuongeza ushiriki wa wanawake katika shughuli za kiuchumi na uzalishaji mali kwa kuzindua Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi. Aidha, majukwaa **116** yamezinduliwa katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na Kata, ambapo jukwaa **1** la Mkoa, majukwaa **7** ya Halmashauri na majukwaa **108** yaKata kati ya Kata **158** yakiwa na lengo kuu la kuelimisha nguzo tisa za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Hali iliyopelekea Mkoa kupata tuzo ya Taifa ya uwezeshaji, kwa kushika nafasi ya kwanza kati ya Mikoa **26** ya Tanzania Bara katika mwaka wa fedha 2016/2017.

## Sekta ya Ushirika

Vyama vya Ushirika 12 vya walaji (Consumers) vimeandikishwa katika Tarafa ya Ngorongoro. Lengo ni kusaidia wananchi kuapata bidha/chakula kwa urahisi na bei nafuu ili kuweza kukabilina na hali ya ukame.

## 3.0. SEHEMU YA MAJI

**Jitihada za kuondoa kero ya upatikanaji MAJI:**
**Maji vijijini.**

- Hadi kufikia Desemba 2016 Hali ya utekelezaji wa miradi ya **vijiji 10** katika halmashauri (***Programu ya Maji Vijijini***) ilikuwa ya kusuasua kutokana na Wakandarasi wengi kusitisha utekelezaji wa kazi za miradi hiyo kutokana na madeni makubwa waliyokuwa wanadai.
- Hali ilivyo sasa Serikali imelipa madeni ya Wakandarasi hao kufikia kiasi cha **Bilioni 2.651**na inaendelea kulipa Wakandarasi wanaohusika kulingana na kadri kazi zinavyofanyika. **Aidha usimamizi kwa sehemu kubwa ya kazi hizo** kwa sasa unafanyika na **wataalamu wa Halmashauri kwa kushirikiana na Mkoa** baada ya wataalamu washauri kujitoa kutokana na madeni waliyokuwa wanadai. Hali ya utekelezaji kwasasa imeongezeka ambapo miradi kumi zaidi imekamilika kutoka **19** mwaka jana hadi kufikia **29** sasa, hivyo watu **143,572** wameanza kupata maji baada ya kusubiri muda mrefu toka miradi hiyo ianze.
- Kwa msukumo huu wa Serikali **tunatarajia** hadi kufikia **Juni 2018** miradi **33** zaidi itakuwa imekamilika na watu takribani **450,000** wataanza kupata huduma ya maji, hali hii itanyanyua upatikanaji wa maji vijijini kutoka asilimia **58.6 sasa** hadi kufikia asilimia **65.**

- Mradi wa vijiji vitano unaochangiwa na Serikali kwa **Bilioni 1.3** na DFID kwa **Bilioni 4.5** umeanza katika halmashauri ya Arusha ambapo tunataraji watu **50,000** zaidi wataanza kupata huduma ya maji hadi kufikia Desemba 2018.
- Huu ni mwendelezo wa kuelekea kwenye lengo la Serikali la kutoa huduma ya maji kwa **85%** vijijini ifikapo 2020.

## 1. Maji Mjini

### i. Maji kwa jiji la Arusha :

- Kuanza kwa mradi mkubwa wa **476 bilioni( chini ya AUWSA mkopo nafuu kutoka AfDB)** :
  Hatua ya Upembuzi yakinifu imekamilika na sasa utekelezaji wa miradi ya kuongeza upatikanaji maji kwa jiji la Arusha kutoka **42.9%** hivi sasa hadi kufikia **100%miaka 2** ijayo umeanza na uchimbaji wa visima **virefu 11** katika shamba la Mbegu (ASA) umeanza na unaendelea mradi huu ulizinduliwa na Mhe. Waziri wa Maji na Umwagiliaji mwezi **Oktoba, 2017**; mradi pia unalenga kuinua huduma ya uondoaji majitaka katika jiji kutoka **7.6%** hivi sasa hadi kufikia **30%** utakapokamilika.

### ii. Maji kwa Mji wa Longido ( Utekelezaji chini ya AUWSA kwa niaba ya Serikali):

- Mradi wa kupeleka majisafi katika mji wa Longido kwa kutokea mto simba uliopo katika wilaya ya **Hai – Kilimanjaro** takribani **km.69** umeanza na unaendelea kujengwa, kiasi cha **16 bilioni** zitatumika na mradi utaondoa tatizo la huduma ya maji kwa mji huu ambao kwa sasa huduma ya maji ni chini ya **20%** hadi kufikia zaidi **ya 85%** hii ni pamoja na vijiji vya *Orbomba, Ranchi na Engikareti*; kwa sasa utekelezaji umefikia **zaidi ya 50%** na inategemewa ifikapo **Juni, 2018** mradi utakuwa umekamilika. Mradi ulizinduliwa na Mhe. Waziri Mkuu mwezi, **Septemba, 2017.**

### Usimamizi wa Huduma za maji katika makao makuu ya wilaya:

**iii.** Kwa sasa Miji mikuu yote ya**wilaya (6)**ina bodi za usamamizi wa Mamlaka zao za maji ukilinganisha na Bodi tano 5 zilizokuwepo kufikia **Desemba 2016**. Aidha pia imeongezeka Bodi ya usimamizi wa Mamlaka ya maji ya **Mji mdogo** wa Ngaramtoni.

- *Wastani wa upatikanaji maji mijini mpaka sasa kimkoa ni 42.9% na lengo ni kufikia 95% kwa miji mikuu ya mkoa na 90% kwa miji ya wilaya ifikapo 2020 kama inavyoelekezwa na Serikali.*
- Utekelezaji wa miradi 2 tajwa hapo juu utainua wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji mijini hadi kufikia 80% ya mahitaji.

**2. Kusogeza huduma za maji kwa wananchi wenye adha kubwa ya huduma ya maji kupitia Mamlaka za Maji :**

- Mamlaka za Maji kwa kiasi kikubwa zimejenga uwezo mkubwa katika kutoa na kuendeleza huduma za maji hata nje ya mipaka yake na kusogeza huduma kwa wananchi wenye uhitaji mkubwa au wanaokabiliwa na adha kubwa ya maji kama ifuatavyo:
  - AUWSA wamesogeza huduma kwa wananchi wa vijiji vya Halmashauri ya Arusha – maeneo ya *Burka, Kisongo na Matevesi*.
  - Mamlaka ya maji Monduli kupitia chanzo chake cha maji inapeleke maji kwa vijiji vya *Meserani Juu* na sasa kuna mradi unaendelea kupeleka maji kwa wananchi wa *Lendikinya* na hapo baadaye *Mtimmoja* na *Nanja* .

## 4.0. KITENGO CHA SERIKALI ZA MITAA

1. Kwa Mwaka 2016/17 Halmashauri za Mkoa wa Arusha zilikusanya julma ya shilingi **27,347,677,414** ikiwa ni asilimia 95% ya makisio 28,909,733,983 waliokuwa wamepanga.Makusanyo hayo yameongezeka kwa asilimia 19 yakilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2015/16 ambayo yalikuwa **22,731,853,820** sawa na asilimia 76 ya makisio ya 29,883,651,008 yaliyokuwa yamepangwa. Ongezeko hili la makusanyo ya ndani ya Halmashauri ni matokeo ya usimamizi mzuri, matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa makusanyo ya mapato ya ndani (Local Government Revenue Collection Information System – LGRCIS) unaotumika katika Halmashauri zote na matumizi ya Points of Sales (POS) katika kila chanzo. Jedwali lifuatalo linaonesha makusanyo kwa kila Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2016/17.

| HALMASHAURI | MAKISIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| ARUSHA CC | 12,299,585,000 | 13,603,884,903 | 111% |
| ARUSHA DC | 3,200,600,000 | 2,944,941,862 | 92% |
| MERU DC | 3,627,024,000 | 3,411,094,173 | 94% |
| LONGIDO DC | 1,343,549,980 | 904,070,011.17 | 67% |
| KARATU DC | 3,887,383,000 | 2,731,081,486 | 70% |
| NGORONGORO DC | 2,094,282,000 | 1,542,484,157 | 74% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| MONDULI DC | 2,415,317,000 | 2,210,120,822 | 90% |
| **JUMLA** | **28,909,733,983** | **27,347,677,414** | **95%** |

Kwa mwaka wa fedha 2017/18 Halmashauri za Mkoa wa Arusha zimekasimia kukusanya jumla ya shilingi 31,642,381,000 kutoka kwenye vyanzo vya ndani. Hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2017 jumla ya shilingi 12,178,915,825 sawa na asilimia 38.49 zilikuwa zimekusanywa. Jedwali lifuatalo linaonesha makusanyo kwa kila Halmashauri hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2017

| HALMASHAURI | MAKISIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| ARUSHA CC | 14,580,000,000.00 | 5,976,702,539.00 | 40.99 |
| ARUSHA DC | 3,493,318,000.00 | 1,304,011,053.00 | 37.33 |
| MERU DC | 3,710,623,000.00 | 1,465,110,295.00 | 39.48 |
| LONGIDO DC | 1,039,747,000.00 | 519,552,217.00 | 49.97 |
| KARATU DC | 2,211,206,000.00 | 906,180,470.00 | 40.98 |
| NGORONGORO DC | 4,177,604,000.00 | 1,268,922,171.00 | 30.37 |
| MONDULI DC | 2,429,883,000.00 | 738,437,080.00 | 30.39 |
| **JUMLA** | **31,642,381,000** | **12,178,915,825** | **38.49** |

2. Mkoa umezisimamia na kuzijengea uwezo Kamati za ukaguzi za Halmashauri na mafanikio yameonekana katika ukaguzi wa Hesabu za Serikali ambapo Halmashauri Tano zilipata Hati Inayoridhisha za Ukaguzi ukilinganisha na mwaka uliopita ambapo ni Halmashauri tatu tu zilipata hati inayoridhisha.

| HALMASHAURI | MWAKA 2014/15 | MWAKA 2015/2016 |
|---|---|---|
| ARUSHA CC | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| ARUSHA DC | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| KARATU DC | Hati isiyoridhisha | Hati yenye mashaka |
| LONGIDO DC | Hati yenye mashaka | Hati yenye mashaka |
| MONDULI DC | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| MERU DC | Hati yenye mashaka | Hati inayoridhisha |
| NGORONGORO DC | Hati yenye mashaka | Hati inayoridhisaha |

3. Hadi kufikia Decemba 2017 Mkoa ulifanikiwa kutoa mafunzo kwenye Nyanja mbalimbali kama vile Utumishi, Fedha na Uchumi kwa Watumishi wa Halmashauri. Mafunzo haya yameboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa Wananchi ukilinganisha na Desemba 2016 ambapo Watendaji wa Halmashauri walikuwa hawajapata mafunzo husika.

4. Halmashauri zote kwa sasa zinatumia mifumo ya Kieletroniki katika kukusanya na kufanya matumizi ya fedha ukinganisha na Miaka iliyopita ambapo Halmashauri zilikuwa zinakusanya kwa kutumia mifumo lakini Matumizi yakifanyika kwa njia ya hundi. Utumiaji wa mifumo umeongeza udhibiti wa mapato na Matumizi.

## 5.0. SEKSHENI YA MIPANGO NA URATIBU

## SEKRETARIET YA MKOA

**1.**Ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri zote 7 umefanyika, na jumla ya miradi 398 kati ya miradi 613 iliweza kukaguliwa kwa kipindi cha Julai hadi Juni 2016/2017.

Seksheni pia imeweza kukagua miradi 125 ya mwaka wa fedha 2017/2018 na mingi ya miradi hii ipo katika sekta za Afya, Elimu, Maji na Barabara. Utekelezaji wa miradi hii upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na baadhi ya miradi imekamilika ikiwemo miradi ya ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu (6 in one), mabweni ya wanafunzi, ujenzi wa vituo vya afya, Zahanati na baadhi ya miradi ya Maji Vijijini

**2**. Uanzishwaji wa jukwaa la wanawake la Mkoa wa Arusha limeanzishwa na sasa wanawake wa mkoa wa Arusha wanazo fursa mbalimbali za kutumia jukwaa hili katika kujikwamua kiuchumi kwa kuanzisha biashara mbalimbali na kupata fursa ya kuunganishwa katika mtandao wa taasisi za kifedha zitakazoweza kuwakopesha kwa riba nafuu sana

**3**. Kwa upande wa programu ya TASAF III na OPEC III mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na

- Mpango wa kunusuru kaya maskini ambapo katika Mkoa wa Arusha Jumla ya Kaya maskini 62,492 zikiwa na wanaume 5,059 na wanawake 41,771 zimeweza kutambuliwa baada ya kukidhi viegezo.

- Jumla ya fedha Tshs 22,652,188,870.37 zilipokelewa katika Mkoa wa Arusha toka TASAF Makao Makuu kwa ajili ya malipo ya Kaya maskini

zipatazo 46,771 katika Vijiji na Mitaa 290 tangu awamu ya kwanza ya mpango huu Julai hadi Agasti 2015

- Mkoa umefanikiwa kutekeleza miradi 63 ya ujenzi wa miundombinu mbalimabali ya Jamii, ikiwemo miradi ya sekta ya elimu, Afya, Barabara, mifereji ya umwagiliaji na mazingira, yenye thamani ya Tshas 2,748,468,978.39 (miradi 9 kwa kila Halmashauri ya Wilaya)

## 6.0. SEKSHENI YA ELIMU

- Uandikishaji wa wanafunzi wa kuanza Elimu ya awali na darasa la kwanza hadi Desemba 2016 ulikuwa wanafunzi **88,268** lakini hadi kufikia Desemba 2017, hali ya maoteo ya uandikishaji wa elimu ya Awali ni wanafunzi **102,411** (**wav 52,142 was 50,269).**

- Mkoa umekuwa na ongezeko la madarasa ya Elimu ya Awali kutoka **647** Desemba 2016, hadi kufikia **715** Desemba, 2017 sawa na ongezeko la **9.23%** shule za msingi **690** Desemba, 2016 hadi shukle za msingi **723** Desemba, 2017 sawa na ongezeko la **4.56%** sekondari **230** Desemba, 2016 hadi shule **213** Desemba 2017 sawa na ongezeko la **0.43%.**

- Uchaguzi wa wanafunzi wa kuanza kidato cha kwanza hadi kufikia mwezi Desemba, 2016 ulikuwa ni wanafunzi **26,984(wav 12,583 was 14,401)** sawa na **100%** ya wanafunzi wote waliofaulu. Uchaguzi wa wanafunzi watakaoanza kidato cha kwanza Januari, 2017 ni **29,624(wav 14,215, was 15,409)** ongezeko la wanafunzi **2,640.** Wanafunzi wote waliofaulu sawa na**100%** wamepata nafasi ya kujiunga kidato cha kwanza 2018.

- Hadi Desemba, 2016 Mkoa ulikuwa na jumla ya shule **118** ambazo zilikuwa hazijasajiliwa na zilikuwa zinaendeshwa kinyume cha sheria ya Elimu Na. 24 ya mwaka 1978 na marekebisho yake ya 1995 na 2002. Lakini hadi kufikia Desemba, 2017 shule zote (**BUBU)** zisizo na usajili zimefungwa na wanafunzi wamehamishiwa kwenye shule zenye usajili.

- Hadi kufikia Desemba, 2016 Mkoa kupitia Halmashauri zake haukuwa na mradi wowote chini mpango wa Lipa kwa Matokeo (P4R) lakini katika kipindi cha mwaka mmoja hadi Desemba 2017 Mkoa ulipokea Tsh. **1,036,000,000/=** kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya shule mpya za kidato cha Tano za Mwandeti, Mlangarini, Nainokanoka na Loliondo na kila shule ilipewa Tsh. **259,000,000/=** za ujenzi wa madarasa, maabara, bweni moja na matundu ya vyoo umekamika 100%. Ujenzi bweni la pili umekamilika kwa 20%.

- Mdondoko wa wanafunzi (Drop out) wa shule za msingi umepungua kutoka **18%** Desemba 2016 hadi kufikia **16%** Desemba 2017 kwa wanafunzi walioanza darasa la kwanza ikilinganishwa na waliomaliza darasa la Saba 2017. Lengo ni kuhakikisha mdondoko unapungua chini ya 10% mwaka 2018 na hatimaye kumalizika kabisa.

- Kupitia Mpango wa Elimu bila Malipo, shule za msingi na Sekondari zimeendelea kupokea wastani wa Tsh. **1,842,990,926/=** kwa mwezi ikiwa ni ruzuku ya uendeshaji wa shule ambapo shule za msingi zinapokea Tsh. **620,091,380/=** na shule za sekondari zinapokea Tsh. **1,222,899, 546/=.**

- Hadi kufikia Desemba 2017 serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa shule ya sekondari na msingi maalum kwa watoto wenye mahitaji maalum. Gharama ya mradi huo ni Tsh**. 4.5** bilion na awamu ya kwanza zimepokelewa Tsh. **1.2** bilioni na ujenzi unaendelea. Lengo ni kuhakikisha ujenzi umekamilika 2018.

- Desemba 2016 vijana **200** waendesha pikipiki (bodaboda) walipewa mkoa wa pikipiki **200** usio na riba zenye thamani ya Tsh. **400,000,000/=.** Kufikia tarehe 27 Desemba, 2017 kiasi cha Tsh. **284,851,644/=** kimekwisha rejeshwa sawa na**66.7%** ya marejesho yote ambayo ni Tsh. **427,140,000/=.** Wastani wa vijana waliorejesha ni **133.4** kati ya vijana **200** na wastani wa vijana ambao hawajarejesha ni **66.6** tu sawa na **33.3%** kati ya vijana **200**. Baada ya kukamilisha marejesho yote Tsh. **200,000,000/=** zitabaki kama mtaji kwa vijana

hawa na Tsh.**200,000,000/=** matarajio ya fedha zilizobaki kwa mwaka 2018 ni kuzielekeza kwa akina mama wamachinga kama mkopo ya mitaji isiyokuwa na riba.

## 7.0. SEKTA YA ARDHI

Katika sekta ya miundombinu mambo muhimumatano (5) yaliyoshughulikiwa ni pamoja na:-

1. Utatuzi wa mgogoro wa Pori Tengefu la Loliondo, mgogoro ulioanza mwaka 1992, mgogoro uliodumu kwa takribani miaka 25 na chanzo kikubwa cha mgogoro ni mgongano wa matumizi ya Ardhi unaotambuliwa na sheria mbili tofauti zinazotumika katika eneo moja yaani ni sheria ya Hifadhi ya Wanyama Pori Na. 5 ya mwaka 2009 na sheria ya Ardhi ya vijiji ya mwaka 1999.

   Hivi sasa serikali imeshatolea maelekezo ya namna ya utatuzi ikiwa ni pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii kuandaa Muswada wa sheria utakowasilishwa serikalini kupitia Baraza la Mawaziri kuhusu sheria Mahsusi ya eneo la Loliondo.

2. **Utatuzi wa migogoro mbali mbali ya Ardhi**

   Mkoa umeshughulikia migogoro ya Ardhi iliyodumu kwa muda mrefu 124 kwa mwaka 2017 kutoka migogoro 42 iliyoshughulikiwa mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 192.2 na lengo ni kuhakikisha migogoro yote inatakyojitokeza mwaka 2018 itatatuliwa kwa wakati**.**

   Aidha katika kutatua migogoro ya ardhi katika Jiji la Arusha jumla ya viwanja 163 vimetolewa kwa wananchi waliokuwa wanadai fidia ya viwanja mbadala katika eneo la Oljoro.

3. **Kutenga maeneo ya uwekezaji na viwanda**

Mkoa kupita Wilaya zake umehimiza kutenga maeneo ya uwekezaji na viwanda na bandari kavu ambapo mpaka hivi sasa jumla ya ekari 215,488.8 zimetengwa kutoka ekari 111,203 mwaka 2016 sawa na ongezeko asilimia 93.7.

Aidha malengo kwa mwaka 2018 ni kuhakikisha maeneo hayo yanawekewa miundombinu na kuhamasisha wawekezaji na kuendelea kutenga maeneo mapya. Maeneo yaliyotengwa kwa kila Halmashauri ni kama ifuatavyo:-

(i) Halmashauri ya Jiji la Arusha ekari 35.4
(ii) Halmashauri ya Wilaya ya Meru ekari 4,000
(iii) Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ekari 125,603.4,
(iv) Halmashauri ya Wilaya ya Karatu 13,888.8
(v) Halmashauri ya Wilaya ya Longido ekari 37.5
(vi) Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro ekari 130.7 na
(vii) Halmashauri ya Wialya ya Monduli ekari 71,793

**Jumla 215,488.8**

4. Kukamilika kwa Mpango Kambambe wa Jiji la Arusha na viunga vyake (Arusha Master Plan) ambapo hivi sasa umewasilishwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kuidhimishwa, Jiji la Arusha lilikuwa na mpango kabambe ambao uliisha muda wake toka mwaka 2016.

5. Upimaji wa maeneo ya Taasisi za Umma, umeongozeka kutoka maeneo 62 mwaka 2016 hadi 134 mwaka 2017 ongezeko lamaeneo 72 sawa na asilimia 116.

## (B) SEKTA YA BARABARA

- Mradi wa Ujenzi wa Barabara kutoka njia mbili hadi njia nne kutoka Sakina hadi Tengeru (14.1km).

- Mradi wa ujenzi wa barabara ya mchepuko wa kusini (By Pass km. 42.41. kwa kiwango cha lami barabara ambayo haikuwepo kwa gharama Tshs.166,.016,742,402.
- Mradi wa ujenzi wa barabara ya Mto wa Mbu – Loliondo (Wasso – Sale Km 49). Kwa kiwango cha lami Wilaya pekee katika Mkoa wa Arusha ambayo haikuwahi kuwa na lami. Mradi umeanza tarehe 18 Oktoba, 2017 na utagharimu Tshs. Billioni 87. Na utachukuwa jumla ya miezi 24 mpaka ukamilike.
- Mradi wa ujenzi wa barabara ya KIA – Mererani kwa kiwango cha lami Km.26 kutoka changarawe umekamilika. Gharama za mradi zilikuwa ni Tshs. Bilioni 32.
- Kijenge – Usa River (Nelsoni Mandela) Ujenzi wa Km.2 kwa kiwango cha lami kwa gharama ya Tshs.Bilioni 1.48 uko mbioni kuanza.
- Ongezeko la Ujenzi wa mtandao wa barabara za Jiji la Arusha kutoka Km.3.10 2016 hadi Km 10.88 mwaka 2017 kwa fedha za msaada wa World Bank.

## 8.0. SEKTA YA AFYA MWAKA 2017

### MAFANIKIO USAFI WA MAZINGIRA

Kwa mwaka 2017 Mashindano yalifanyika kote nchini kwa kushirikisha ngazi ya Halmashauri za Wilaya,Manispaa, miji, Majiji, vijiji,Hospitali za Rufaa za Serikali na za binafsi pamoja na Hotel zenye hadhi ya nyota tano.

Mkoa ulifanya vizuri na kushinda tuzo zifuatazo:-

i. Katika Ngazi ya Halmashauri za Wilaya, Halmashauri ya Meru ilishinda nafasi ya kwanza na kuzawadiwa gari mpya aina ya Nissan Patrol
ii. Ngazi ya Halmashauri za manispaa na majiji, Jiji la Arusha ilishinda nafasi ya pili nakuzawadiwa cheti na pikipiki 2 aina ya Yamaha
iii. Ngazi ya Hoteli za kitalii, Hoteli ya Mount Meru ilishinda nafasi ya pili nakuzawadiwacheti .
iv. Ngazi ya Hospitali za Rufaa za binafsi na za Serikali za Mikoa-
    - ALMC- nafasi ya kwanza- zawadi ya cheti cha ushindi nafasi ya kwanza
    - Hospitali ya Rufaa ya Mount Meru mshindi wa tatu- zawadi ya cheti cha ushindi nafasi ya tatu
v. Ngazi ya Vijiji bora ni Kijiji cha Nambala- Meru DC- nafasi ya pili kitaifa – zawadi ya pikipiki mpya aina ya Yamaha.

Tupo kwenye mchakato wa kuendeleza dhana ya ushindi kwa kupanga mikakati ya kudumu kuendelea kuwa washindi.

## USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI NA ZA SERIKALI (PPP)

Mkoaunatambua mchango mkubwa wa Wadau katika kuboresha huduma za Afya katika Halmashauri zetu na kukabiliana na majanga mbalimbali.

Katika mwaka wa fedha wa 2016/17 Mkoa kwa kushirikiana na Mdau wa Afya Leopard Tours and Safaris' waliweza kukarabati jengo la kupimia wingi wa Virusi vya UKIMWI (Viral Load)katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ambalo limeshaanza kutoa huduma hivyo na kupelekea wagonjwa wanaotumia dawa kujua matokeo mapema na kupunguza gharama za usafirishaji wa sampuli kwenda KCMC. Mkoa pia unapokea sampuli kutoka Mikoa jirani ya Manyara na Singida. Hadi kufikia Desemba, 2017 idadi ya wagonjwa wa UKIMWI waliopimwa kwa kutumia vipimo vya Viral Load.

### Uibuaji wa wagonjwa wa Kifua Kikuu

Kupitia ufadhili wa NTLP,Mkoa umeweza kuchagua Maduka ya dawa binafsi na kuyajengea uwezo wa kutambua dalili za mwanzo za kifua kikuu ili kuwapa rufaa kwenda kwenye maabara binafsi zilizoteuliwa kupima makohozi kwa lengo la kuongeza kasi ya kuibua wagonjwa wa Kifua kikuu mapema. Jumla ya maduka 13 na maabara 5 zinatoa huduma hiyo.

Kupitia ufadhili wa KNCV,Mkoa umefanikiwa kuongeza uibuaji wa wagonjwa wa kifua kikuu mfano wamefanikiwa kuweka darubini ya kisasa (LED-Fluorence Microscopy) katika Halmashauri ya Longido na kupekelea kuongeza idadi ya wagonjwa kutoka 14 mpaka 61.Pia wameweka machine ya kisasa yenye uwezo wa kugundua vimelea vya kifua kikuu na usugu wa dawa za kifua kikuu (GXP-GeneXpert) amabayo imeweza kuibua wagonjwa wengi zaidi.

## HUDUMA ZA MAMA NA MTOTO

### A: Ukarabati wa vyumba vya cPAC

- Katika kupambana na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, kwa kushirikiana na wadau Engenderhealth wamesaidia kukarabati vituo 16 kati ya vituo 52 vinavyotoa huduma baada ya mimba kuharibika.
- Ujenzi wa vyumba vya upasuaji 3 katika vituo vya kutoa huduma za Afya vimekamilika na kuanza kazi.

## UUNDWAJI WA TIMU YA URATIBU WA AFYA MOJA "ONE HEALTH COORDINATION TEAM"

Mkoa wa Arusha umefanikiwa kuanzia Timu ya Afya moja (*One health coordination team)* inayoshirikisha sekta mbalimbali katika kukabiliana na magonjwa mbalimbali

mfano magonjwa yanayoweza kuenezwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu kama kimeta, magonjwa yanayohusisha maji kama kipindupindu na majanga mengine yanayosababisha madhara kwa afya ya binadamu. Tumefanikiwa kuelimisha jamii kuhusiana na magonjwa ya mifugo yanayoenezwa kwa binadamu, kuchukua sampuli 27 za binadamu kwa uchunguzi wa maabara wa kimeta ambapo 7 zilithibitishwa. Pia Mkoa umefanikiwa kutoa chanjo kwa mifugo 405,462(7%) kati ya mifugo 5,760,329.

**UTOAJI WA TAARIFA YA MAGONJWA KWA NJIA YA KIELEKTRONIKI**

Mkoa wetu umefanikiwa kutuma ripoti kwa ukamilifu kwa wastani wa asilimia 94 na kwa wakati asilimia 75 kwa mwaka 2017.

**TAARIFA YA MAFANIKIO YA TAKWIMU (MTUHA)**

- Tumefanikiwa kushika nafasi ya nne ngazi ya Kitaifa katika uingizaji wa takwimu kwa wakati na usahihi (Jan-Jun 2017)
- Mkoa umefanikiwa kushika nafasi ya kwanza kitaifa katika utoaji wa taarifa za mwenendo wa kulaza wagonjwa (Bed Occupancy) kwa wakati na usahihi kwa mwaka 2017

**MAFANIKIO MAKUBWA KATIKA HOSPITALI YA MOUNT MERU**

**Ununuzi wa mashine ya kisasa ''Ultra-Modern Ultra sound with Dopler''**

Mkoa kwa kushirikiana na Mdau wa Afya kutoka Netherland wameweza kuinunulia Hospitaliya Mkoa ya Mount Meru ''Ultra-Modern Ultra sound with Dopler'' yenye thamani ya Tsh.40,000,000/= ambapo inapima vipimo vifuatavyo:-

- Magonjwa na mapungufu mbalimbali ya mishipa ya damu (Deep Venous thrombosis)
- Kusinyaa kwa mishipa ya damu (Atherosclerosis)
- Upimaji wa matiti (Uvimbe na saratani)
- Kupima viungo vyote vya ndani ya mwili
- Kupima hali ya ubongo kwa watoto baada ya kuzaliwa.

Kutokana na mashine hii, Hospitali yetu imeweza kupunguza kutuma wagonjwa nje kutafuta vipimo hivyo na kuongeza idadi ya wagonjwa wanaohitaji vipimo hivi kutoka nje ya Hospitali. Vile vile tumeweza kuongeza mapato kutoka shilingi 1,228,587,852/= (2015/16) hadi 1,776,564,311 (2016/17) sawa na ongezeko la 45%.

## 9.0. KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI (RS)

Mambo Matano ya ufanisi katika Kitengo Cha Ukaguzi wa Ndani – Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha ni yafuatayo;

1. Kitengo kimeweza kufanya ukaguzi katika kipindi hicho na kufanikiwa kutoa taarifa za kila robo mwaka kwa mujibu wa Sheria, Taratibu na Maelekezo mbalimbali ya Serikali. Hali hiyo imeimarisha usimamizi wa rasili mali za umma na utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika sekretarieti ya Mkoa wa Arusha. Taarifa hizo ni zifuatazo:
    - Taarifa ya Ukaguzi kwa robo ya Kwanza 2016/2017 (Julai-Septemba, 2016)
    - Taarifa ya Ukaguzi kwa robo ya Pili 2016/2017 (Oktoba-Desemba,2016)
    - Taarifa ya Ukaguzi kwa robo ya Tatu 2016/2017 (Januari-Machi. 2017)
    - Taarifa ya Ukaguzi kwa robo ya Nne 2016/2017 (Aprili-Juni, 2017)
    - Taarifa ya Ukaguzi kwa robo ya kwanza 2017/2018 (Julai-Septemba, 2017)

2. Kitengo kimeweza kuhakiki Madai mbalimbali ya Watumishi, Wakandarasi, wazabuni na Watoa huduma ambayo kwa kiwango kikubwa yalikubalika na kulipwa kwa kiasi kikubwa pia.

3. Kitengo kimeweza kushiriki kikamilifu zoezi la upitiaji na uchambuzi wa majibu ya hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2015/2016 kwa Halmashauri zote saba za Mkoa wa Arusha, na Ushauri ulitolewa ipasavyo.

4. Kitengo kimeweza kushiriki kikamilifu katika zoezi la upimaji wa awali 'Mock Assessment'. Zoezi ambalo linazipima Halmashauri kuona kama zimefanya maandalizi kwa ajili ya kukidhi vigezo vya kupatiwa fedha za ruzuku ya maendeleo (LGDG)

## 10.0. KITENGO CHA TEHAMA

Mafanikio katika mwaka 2017 kitengo cha TEHAMA.

1. Kusimika Mfumo wa Uendeshaji na Usimamizi wa Vituo vya Kutolea huduma za Afya (GoT- HoMIS) katika Hospitali ya Mkoa na za wilaya za Mkoa wa Arusha, ambazo ni;
    - *Hospitali ya Wilaya ya Arusha (Oltrument).*
    - *Hospitali ya Wilaya ya Meru,*
    - *Hospitali ya Wilaya ya Monduli*
    - *Kituo cha Afya Karatu.*
    - *Kituo cha Afya Waso (Ngorongoro Dc)*
    - *Kituo cha Afya daraja mbili (jiji)*

Kwa upande wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na vituo vya afya mapato yameongezeka kwa marambili zaidi ukilinganisha na kipindi cha awali kabla ya kutumia mfumo.

2. Kusimamia usimikwaji wa Mtandao Kiambo (LAN), Mtandao Mpana (WAN) na Mawasiliano ya Ndani ya simu za mezani (PBX) katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,

Halmashauri ya Jiji la Arusha, Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mt. Meru chini ya Mradi wa GovNet.

3. Kusimamia usimikwaji wa Mfumo wa mahudhurio "Biometric Time and Attendance Monitoring System" umesaidia kuongeza ufanisi wa kazi kama watumishi kuwahi kazini, kuacha utoro pia mfumo umesaidia kuboresha utoaji wa huduma, nidhamu kwa watumishi.

4. Kusimamia maboresho ya Website ya Mkoa (www.arusha.go.tz) na matumizi wa email za serikari (GMS- Government Mailing system)

## 11.0.KITENGO CHA UHASIBU

1. Kutoka na kitengo kutekeleza vizuri kazi zake tumeweza kuiletea hati safi ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

2. Kutokana na utunzaji mzuri wa kumbukumbu za madeni kwa mwaka ulioishia 2016/2017 Mkoa umeweza kupatiwa fedha za madeni kiasi cha shilingi 2,033,496,410.00 na kuweza kulipa madeni ya watumishi,wazabuni na wakandarasi.

3. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kupitia kitengo chake cha uhasibu imekuwa ikiwajali watumishi wake na kuhakikisha wanapata stahili zao kwa wakati pindi fedha zinapokuwepo bila usumbufu.ikiwa Extra duty kwa watumishi wa kada za chini,utilities kwa viongozi,fedha za likizo, Stahili za Madaktari na wauguzi na stahili nyinginezo.

4. Kwa kutumia mtandao wa malipo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imeweza kuwezesha ulipaji wa malipo wa moja kwa moja kwenye Akaunti za watumishi na wazabuni kwa njia ya TISS na kuondoa usumbufu wa kwenda na hundi Benki.

5. Kwa kutumia Mtandao wa malipo utengenezaji wa Hesabu za Mwaka umerahisishwa na hesabu zinapatikana kwa wakati na bila usumbufu.

### 12.0 HITIMISHO

Tangu Serikali ya awamu ya tano ilipoingia madarakani Novemba 2015 imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015 – 2020, kama Mkoa mambo mengi

yatatekelezwa katika kuinua uchumi, ujenzi wa miundombinu, uboreshaji wa huduma za Afya, Elimu, Ukusanyaji wa mapato na utumiaji sahihi wa mapato ya Serikali.

Lengo ni kumsaidia mwananchi mnyonge na kuboresha maisha ya jumla ya wananchi kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Jukumu la wananchi ni kuunga mkono juhudi za Serikali chini ya Uongozi wa Rais John Pombe Magufuli na wasaidizi wake wote.

MRISHO MASHAKA GAMBO
**MKUU WA MKOA**
**ARUSHA**